*Re-aranged and translated by Pastor Stephen Letta*

## Yohana Kajembe Mseli, (1883 – 1983)

Yohana Kajembe Mseli alikuwa mmoja wa waumini sita wa kwanza wa Waadventista wa Sabato nchini Tanzania. Kisa cha maisha yake kinaonyesha baadhi ya mapambano ya Waadventista wa awali katika nchi ya Tanzania ambayo wakati huo ilifahamika kama Tanganyika.

### Kuzaliwa na Kubatizwa

Yohana Kajembe Mseli alizaliwa mwaka 1883 katika kijiji cha Mamba Miyamba, Kilimanjaro, nchini Tanzania. Baba yake Mseli, alikuwa kutoka kabila la Wapare, ukoo wa Wajema, ambao wanaaminika kuhama kutoka Taita, Kenya, hadi Tanzania. Kajembe Mseli na wengine watano walikuwa Watanzania wa kwanza kubatizwa mwaka 1908.

### Ndoa

Kajembe hakupata elimu yoyote rasmi. Utoto wake aliutumia huko Mamba Miyamba na akawa mkulima mdogo, akichunga mifugo. Kwa sababu ya mandhari ya milima ya Mamba Miyamba, aliamua kuhamia kijiji cha Kihurio sehemu ya Lukuta, ambayo iko kwenye uwanda wenye rutuba. Katika eneo jipya, Kajembe alimuoa Maria Juma ambaye alizaa naye watoto watatu: Mshinwa Kajembe, Mseli Kajembe, na Namwai Kajembe.

### Kubatizwa

Mnamo 1905, mmishonari wa Kijerumani aitwaye B. Ohme alitumwa Kihurio Lukuta kujenga shule. Katika mchakato wa ujenzi, Ohme alimwajiri Kajembe Mseli kama mpishi. Wakati huo, Kajembe alikuwa tayari amekubali imani ya Kiislamu, lakini Ohme alianza kumhubiri Kajembe na mwaka 1908, baada ya miaka mitatu, Kajembe na watu wengine watano walibatizwa huko Giti na mmishionari wa Kijerumani aitwaye, AC Enns. Baada ya ubatizo alipewa jina la Yohana Kajembe. Mnamo mwaka 1909, ubatizo wa pili nchini Tanzania ulifanyika na watu wengine watano walibatizwa, miongoni mwao ni mke wa Mseli, Maria Yohana Kajembe.

Baada ya kubatizwa, Kajembe alikuwa muumini mwaminifu wa kanisa la Kihurio Mission kwa muda, akiwa na ofisi ya kanisa. Hata hivyo, mke wake Maria aliposhindwa kupata watoto zaidi, alichukua mke wa pili. Mke wa pili aliitwa Namarigo. Kanisa lilimchukulia hatua za kinidhamu na kumuondoa katika ushirika wa kanisa. Hatimaye Kajembe alijiunga tena na imani ya Kiislamu. Namarigo alifariki baada ya kujifungua watoto wawili wa kike.

Baada ya kifo chake, Kajembe alirudi katika kanisa la Waadventista Wasabato Kihurio na kubatizwa tena. Aliendelea kuwa mshiriki mwaminifu wa kanisa la Waadventista hadi alipofariki Septemba 9, 1983, akiwa na umri wa miaka 100. Alizikwa Misheni ya Kihurio.